

SABABU ZA WANAFUNZI WA SHULE ZA
UPILI KUTOFAULU KATIKA SOMO LA
LUGHA YA KISWAHILI KATIKA MJI WA
NANYUKI, KAUNTI YA LAIKIPIA.

JOHN MWAMBURA M.

E35S111/07057

TASNIFU ILIYOWASILISHWA
KUTIMIZA SEHEMU YA MAHITAJI YA
YA SHAHADA YA; BACHELOR OF
EDUCATION (ARTS)

JULAI 2015

SURA YA KWANZA

1:0 Utangulizi

Utafiti wangu unahusu sababu mbalimbali zinazosababisha Wanafunzi wa shule za upili kutofaulu katika somo la lugha ya Kiswahili katikamitihani yao ya kitaifa na hata katika mijarabu mingi wafanyayo mashuleni.

1:1 IKISIRI

Utafiti wangu unahusu sababu mbalimbali zinazosababisha Wanafunzi wa shule za msingi na za upili kutofaulu katika somo la lugha ya Kiswahili. Katika utafiti wangu, nimeangazia Lugha kwa ujumla, historia na chimbuko la Kiswahili na maendeleo yake hapa nchini Kenya. Nimeendelea zaidi na kueleza sajili mbalimbali za lugha. Na hatimaye changamoto zinazoikumba Lugha ya Kiswahili na mikakati ya kuimarisha Kiswahili humu nchini. Sababu ya kuangazia vipengele vilivyotajwa hapo juu ni kuwa, sharti ieleweke mahali Kiswahili kilitoka, kilivyoendelea na changamoto zake, ili iweze kubainika wazi kwa nini Wanafunzi hawafanyi vyema katika somo la Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ni Lugha ya taifa na moja wapo wa Lugha rasmi hapa nchini. Hivyo basi, wanafunzi wanafaa kuwa wakifanya vyema zaidi katika somo hili. Hata hivyo, hali ni tofauti kwani wengi hawalipendi somo hili, hivyo kupata alama duni katika mitihani yao. Nitadokeza pia kwa kifupi lahaja mbalimbali za Kiswahili zinazotumiwa na watu wengi wakiwemo Wanafunzi, ambazo huenda zikachangia katika kuathiri matumizi ya Kiswahili.